

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SABA

27 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 27 APRILI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa

Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

139. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mhe. Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara yenye km 13 kuanzia Rau Madukani – Mamboleo – Shimbwe Juu katika Jimbo la Moshi Vijijini.

140. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIAS NJAU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la mafuriko katika maeneo ya Mbweni Teta, Bunju Basihaya, Kunduchi, Nyamachabes, Ununio na Mikocheni katika Jimbo la Kawe.

141. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mwaka 2015 wakati wa Kampeni, Mhe. Rais aliahidi kujenga barabara ya km 3 katika Mji wa Kakonko ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya:-

Je, kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa na ni lini sasa itatekelezwa.

WIZARA YA KILIMO:

142. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-


Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliingiza Zao la Parachichi katika mazao ya kimkakati kutokana na Zao hilo kuingizia nchi Fedha za Kigeni.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

143. MHESHIMIWA AUGUSTINE VUMA HOLLE (KASULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na mgogoro wa ardhi wa muda mrefu baina ya Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu na Kata ya Makere:-

• Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro huo. •



WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

144. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni gharama kiasi gani na taratibu gani hutumika ili kupata huduma za ulinzi za SUMA JKT.

WIZARA YA MADINI:

145. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wananchi wa Jimbo la Ngara wananufaika na uchimbaji wa Madini ya Nickel unaotarajia kuanza katika eneo la Kabanga.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

146. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni kwanini Serikali haitumii risiti za kielektroniki inapotoza faini za kuingiza Mifugo kwenye Hifadhi zilizopo Sikonge.

147. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Sehemu kubwa iliyokuwa ikitumika kwa shughuli za uchumi katika Wilaya ya Malinyi imetwaliwa na Mamlaka ya

Wanyamapori Tanzania (TAWA) Mwaka 2017; ambapo waliweka mpaka maarufu kama “TUTA LA 2017” bila kushirikisha Wananchi.

Je, Serikali haioni haja ya kurejea na kufanya upya mapitio shirikishi ya mipaka ya eneo hilo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
27 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**